Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# MAJADILIANO YA BUNGE

___________

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Pili – Tarehe 13 Juni, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Nane. Katibu hatua inayofuata.

## MASWALI NA MAJIBU

Na.11

### Maamuzi ya Mji Mdogo wa Mugumu kuwa Halmashauri ya Mji

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE** aliuliza:-

Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* kilichokaa tarehe 8 Machi, 2011 pamoja na mambo mengine kilipitisha uamuzi wa Mji Mdogo wa Mugumu kuwa Halmashauri ya Mji kamili:-

(a) Je, kwa nini hadi sasa hakuna majibu yaliyotolewa wakati vigezo vyote vinavyotakiwa vimetimizwa?

(b) Je, kwa nini mapendekezo ya mgawanyo wa Tarafa, Kata, Vijiji na Vitongoji pamoja na usafiri wa maeneo hayo hayajatolewa?

(c) Je, kwa nini ajira za Watendaji wa Kata na Vijiji hazijatolewa licha ya Halmashauri ya Wilaya kuwasilisha maombi hayo muda mrefu jambo linalozorotesha usimamiaji wa kazi na maendeleo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), imekwishapitia na kuchambua vigezo vilivyowasilishwa na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu ili kuweza kutoa uamuzi wa kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji. Baada ya kupitia vigezo na taarifa hizo, bado Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imetakiwa iwasilishe taarifa inayoonesha matumizi ya sasa ya ardhi iliyopo na inayoweza kutumiwa kwa ajili ya upanuzi wa Mji endapo pendekezo la kupandishwa hadhi litapita ikiwa ni pamoja na nguvu kazi iliyopo na jinsi zitakavyoneemeka au kuathirika na upandishwaji hadhi kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu. Baada ya hapo, Wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), watafika Mugumu ili kukagua vigezo vyote muhimu kabla ya kutoa mapendekezo ya kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya vigezo iliyowasilishwa haikueleza ukubwa wa eneo la Mji Mdogo wa Mugumu na ukubwa wa eneo lote la Halmashauri ya Mji Mpya unaopendekezwa. Aidha, mapendekezo ya Tarafa zitakazojumuishwa kwenye Halmashauri ya Mji Mpya hayajafika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Mapendekezo ya Kata na Vitongoji kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mugumu yalishafanywa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali (Na.173) la tarehe 7 Machi 2010.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuajiri ulibadilika toka Julai, 2010 ulipohamishia mamlaka hayo kwenye Sekretarieti ya Ajira. Ingawa mamlaka za Serikali za Mitaa zimerejeshewa mamlaka ya kuajiri watumishi wa kada ya chini wakiwemo Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji, kinachosubiriwa ni kukamilika kwa mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Ajira ili utekelezaji wa mabadiliko hayo uweze kufanyika.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Katika kufuatilia suala hili la upandishaji hadhi wa Mji Mdogo wa Mugumu kuwa Halmashauri ya Mji, mwaka jana wapo watumishi waliokuja TAMISEMI wakaambiwa kwamba Wataalam wa TAMISEMI watakwenda Halmashauri ya Serengeti lakini mpaka leo hii ujumbe huu wa TAMISEMI haujakwenda. Napenda Naibu Waziri aniambie ni lini ujumbe huu utakwenda?

(ii) Kuhusu suala la ajira, mwaka jana Halmashauri yetu ilileta maombi ya ajira kwa nini kibali hakikutolewa katika ajira ambazo niliona kwenye mtandao, nafasi 533 kwa ajili ya Watendaji wa Vijiji na wa Mitaa, Halmashauri ya Serengeti haimo? Napenda nipate majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme kwamba, hili jambo analolizungumza tutaangalia Dkt. Kebwe hapa wala halina matatizo na kwa vile nilijua kwamba anaweza akali-*raise* hili, ninayo barua hapa ambayo inatoa maelekezo kwamba watuletee hizo takwimu ambazo nimezisema. Nitakuomba uniruhusu baada ya kumaliza kikao hiki nimkabidhi Dkt. Kebwe hiyo barua, kwa sababu barua ilishakwenda na nilijua kwamba italeta matatizo hapa. Barua hii hapa, nitakupa uende nayo, ni kama nakala. Tuletee hiyo, tukishapata hizo takwimu Mheshimiwa Hawa Ghasia, yupo hapa ndiyo kiongozi wetu wa Wizara na Waziri Mkuu yupo hapa, mara moja tutapeleka watu kule wakacheki hii inayozungumzwa. Kwa hiyo, usiumize kichwa chako, hili ni jambo dogo sana ni kama vile limekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili la ajira linalozungumzwa hapa tuelewane vizuri, utaratibu uliokuwepo wa mwanzo ulikuwa mpaka wapishi, wanaofagia, walinzi na korokoroni, wote tulikuwa tunaomba kibali kutoka Tume ya Ajira, ikapigwa kelele hapa tukalalamika, Wabunge wakazungumza hapa na Serikali ikaridhia kwamba kada hizo zote ninazozitaja na zile nyingine za Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata, sasa zirudi tena katika Halmashauri na hilo limeshakubalika. Kinachotakiwa hapa ni kwamba, kwa vile walikwenda kule kwa sheria watarudi tena huku kwenye mamlaka hii kwa sheria. Kwa hiyo, ipo kazi inatakiwa kufanyika hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili analozungumza Mheshimiwa Dkt. Kebwe, waliomba kibali na kwa sababu hata huu utaratibu kama utatoka siyo kwamba Halmashauri zitakwenda kuajiri tu kama tunavyotaka ni lazima kuwepo na *control* kwa sababu mambo yote yanalindwa na bajeti ya hapa. Kwa hiyo, naomba ajue kwamba sisi tutafuatilia hili la kibali na tutaangalia utaratibu wote ili tuweze kuwaruhusu kadiri itakavyokuwa imeruhusiwa kule, siyo kwamba kila mtu atakwenda kuajiri kama anavyotaka. Hili nalo nataka nimthibitishie wala asiwe na wasiwasi, nikimaliza kujibu hapa tukutane mara moja tuzungumze tumalize hii habari.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mwaka juzi Serikali ilitangaza kuanzishwa kwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu lakini hadi leo hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea. Naomba Serikali itoe kauli ni lini Halmashauri ya Mji wa Kasulu itaanza rasmi ili kuanza kusogeza huduma karibu kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Machali, wala siyo yeye tu, zipo Halmahauri nyingi ambazo tulikuwa tumesema na Mamlaka za Mji; kuna Kahama, Masasi, Nzega na nyingine nyingi ambazo tulikuwa tumeshatamka. Naomba avute subira tu, wakati Waziri atakapokuja hapa kwa ajili ya Hotuba ya Bajeti, ambayo nitakuomba haraka haraka uipitishe kwa sababu usipoipitisha sasa ndiyo tatizo litakuwa kubwa, Waziri Mkuu atazungumza hapa, mtasikia hao wote na wale wengine wote mnaosubiri wala msiamke tena kuniuliza swali, hiyo *package* yote itakuwepo kwenye Hotuba ya Waziri.

Na. 12

**Fedha za Ukarabati wa Barabara za Jiji la Mwanza**

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI (K.n.y. MHE. HIGHNESS S. KIWIA)** aliuliza:-

Mvua zilizonyesha mwaka jana ziliharibu kabisa miundombinu ya barabara katika Jiji la Mwanza na kulazimu kuomba kiasi cha shilingi bilioni moja nukta mbili kutoka katika Mfuko wa Dharura wa Serikali kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizo na Serikali ikatoa shilingi milioni mia sita zilizobaki ili kukamilisha kazi hiyo:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari sasa kumalizia kiasi cha shilingi milioni mia sita zilizobaki ili kukamilisha kazi hiyo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya *Mwanza Airport - Kanyenze By Pass?*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Ilemela, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri ya Jiji la Mwanza iliwasilisha ombi la kupatiwa fedha za dharura ili kutekeleza mpango wake wa matengenezo ya dharura kwenye barabara ambazo ziliharibiwa na mvua nyingi iliyonyesha Jijini Mwanza. Mpango wa dharura ulikisiwa kiasi cha shilingi 1,169,000,000, ambapo fedha hizi ziliombwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), zikiwa nje ya makisio ya Bajeti ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Fedha zilizotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ni shilingi 600,000,000 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zifuatazo:-

(i) Pamba (0.6 km) 74mil;
(ii) Posta ‘A’ Mabatini (0.6km) 50 mil;
(iii) Nyakato North (1km) 30 mil;
(iv) Igogwe - Igombe (9 km) 65 mil;
(v) Kamanga By Pass na Hesawa (0.6) km 21 mil; na
(vi) Bigbite - Michungwani (5 km) 360 mil.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kilichotolewa ndicho kilikuwa uwezo wa Serikali ukizingatia kuwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza ndiyo ilipatiwa kiasi kikubwa cha fedha kuliko Halmashauri zote nchini. Ili kukidhi haja kwa barabara ambazo hazikufanyiwa matengenezo, Halmashauri ya Jiji la Mwanza katika Awamu ya Tatu ya Mpango *(Tanzania Strategic Cities Programme - TSCP),* kutumia vyanzo vyake vya ndani katika mpango wake wa bajeti, itatumia jumla ya shilingi 906,702,500.00 kuzifanyia matengenezo barabara hizo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kufanya tathmini ya fidia katika maeneo husika ya Barabara ya Mwanza Aiport - Kayenze By Pass, Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa cha tarehe 3 Juni, 2012 kimeagiza Halmashauri zote katika Mkoa kuleta maombi maalum ya kupandisha hadhi barabara hizi ili zijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara ya Mwanza –Airport –Kayenze By Pass ni mojawapo ya barabara zilizo kwenye utaratibu wa maombi ya kupandishwa hadhi ili hatimaye zijengwe kwa kiwango cha lami.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

(i)Kwa kuwa Barabara ya Mwanza Air Port - Kayenze By Pass inazunguka Uwanja wa Ndege wa Mwanza; na kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Mwanza umesaini mkataba wa kuupanua kutoka mita elfu tatu hadi mita elfu tano; na kwa kuwa Barabara ya Kayenze By Pass inakwenda kumezwa na uwanja huo. Je Serikali haioni kwamba ina kila sababu za makusudi za kuupanua huu Uwanja kwa haraka sana ili kuwawezesha Wananchi wa Kayenze kupata njia mbadala ya kuweza kuwafikisha Mwanza Mjini?

(ii) Kwa kuwa swali la msingi la Mheshimiwa Hoghness Kiwia linafanana kabisa na Barabara ya Nansio - Rugenzi - Kisorya hadi Bunda ambayo imeharibiwa kwa kiasi kikubwa na mvua kiasi cha kuwafanya Wananchi wa Bunda kwa Mheshimiwa Wasira wasiweze kufika Kisorya. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuisaidia hii Barabara ili wananchi waweze kupata huduma za kuingia Ukerewe na kutoka kwenda Bunda?

**NAIBU SPIKA:** Hilo swali la pili umepandia kwa sababu ni la *TANROADS* wakati swali la msingi linahusu barabara ambazo zipo ndani ya Manispaa. Naibu Waziri kwa swali la kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, hili la pili nakushukuru kwamba umenisaidia ndiyo jibu lenyewe na Kiti hiki ninakiheshimu sana. Mimi nadhani hili swali linahusu hawa wenzetu wa *TANROADS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili la kwanza ambalo ameliuliza hapa na hawa wenzetu wamekaa katika Halmashauri ya Jiji, jana nilikuwa nazungumza na Kabwe na wale ambao wana-*doubt* mnaweza mkampigia Kabwe mkamwuliza hivi Mwanri alizungumza na wewe. Mimi nilikuwa nauliza swali analoniuliza hilo, lakini wamekaa wamepitisha hii barabara na wametoka hapo wamekwenda kwenye *Regional Consultative Committee,* sasa *whether* wapo *right* au hawapo *right, I must confess* kwamba sijampata vizuri anachotaka kukipata hapa ni nini, lakini ni jambo ambalo limezungumzwa mle ndani na hao akina Kiwia wapo mle kwenye zile Kamati. Kwa hiyo, kama kuna tatizo lolote tunaweza tukazungumza nikajua ni nini alichozungumza, lakini vikao vyote vimepitisha na hata mambo ya *compensation* na nini yote yamezungumzwa kwenye kile kikao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Mbunge anafikiri sijampata vizuri, nikitoka hapa nipo tayari kuzungumza naye aniambie vizuri anachotaka ni nini, lakini vikao vyote vimekaa, *Regional Consultative* wamekaa na bajeti zote zimepita. Wanachosema katika hii barabara ni kwamba, wanaomba kibali ipandishwe hadhi ili iwe chini ya *TANROADS.* Mwenye mamlaka ya kutoa kibali hicho siyo Waziri wa TAMISEMI, mwenye mamlaka ni Waziri wa Wizara ya Ujenzi, ndiye anayesema hizi barabara zimepandishwa au hazijapandishwa.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa swali la msingi linafanana na tatizo lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ambayo mwaka jana iliomba maombi maalum kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Kalambanzite –Ilemba ya shilingi bilioni mbili lakini Serikali ilitoa milioni mia nne ambazo zilishaanza kutengeneza hizo barabara; ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kukamilisha barabara hiyo na kumalizia hicho kiasi cha fedha kilichobakia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nitahitaji kupata muda kidogo ili nicheki hizi takwimu na kiasi

kilichokwenda nijue tumekwama wapi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge anipe nafasi, kesho asubuhi nikiamka nitakuwa na barua mkononi ikionesha ni nini kilichotokea, kiasi kilichokwenda na kilichobaki. Kesho asubuhi atapata.

Na. 13

**Kitengo cha Utafiti wa Maji Chuo Kikuu cha Nelson Mandela**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MHE. HERBERT J. MNTANGI)** aliuliza:-

Teknolojia inayotumika kutafiti uwepo wa maji ya ardhini kabla ya uchimbaji wa visima virefu imepitwa na wakati na ni ya gharama kubwa mno, na kwa sababu Chuo Kikuu cha Nelson Mandela - Arusha kina Kitengo cha Utafiti wa Maji Ardhini:-

Je, kwa nini Serikali isikikabidhi Chuo hicho jukumu la utafiti wa maji wa kisasa ili kuwezesha upatikanaji maji wa uhakika na kwa gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ya utafiti wa maji chini ya ardhi bado haijabadilika ulimwenguni kote, kinachobadilika ni teknolojia ya vifaa vinavyotumika kufanya utafiti. Utaratibu unaotumika; kwanza ni kujua aina ya miamba iliyopo na hali ya upatikanaji wa maji chini ya ardhi katika eneo husika kwa kusoma taarifa na ramani za kihaidrolojia zilizopo. Hatua hii hufuatiliwa na kufanya utafiti kwa kutumia vifaa vyenye uwezo wa kubaini uwezekano wa kuwepo kwa maji kwenye aina ya miamba iliyopo. Hatua hii haitoi uhakika wa kuwepo kwa maji isipokuwa huonesha uwezekano wa kupata maji kwa kati ya asilimia 50 na 70. Hatua inayofuata ambayo ni ya uhakika ni kuchimba kisima cha uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miongo miwili iliyopita, kumekuwepo na maendeleo makubwa katika kuboresha vifaa vinavyotumika kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi. Vifaa vya sasa vina mfumo wa kompyuta ambao unarahisisha uchambuzi wa takwimu na kutoa majibu ya uhakika zaidi ukilinganisha na vifaa vya miaka iliyopita. Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, ilinunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi. Vifaa hivyo ni pamoja na *Resistivity Meter, Seismic Instrument, Proton Precision Magnetometer* na *Borehole logger*. Vifaa hivi vimesambazwa katika ofisi zote za Maji za Mabonde nchini na visima katika kila bonde. Aidha, Serikali katika kukabiliana na upungufu wa wataalam wa maji chini ya ardhi wenye uzoefu, imeanza kutoa mafunzo kwa wataalam walioajiriwa hivi karibuni. Lengo ni kuwezesha utoaji ushauri sahihi kwa wadau kuhusiana na utafiti na uendelezaji maji chini ya ardhi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Vyuo Vikuu na Taasisi zingine za Elimu ya Juu ni pamoja na kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri elekezi *(consultancy)* katika masuala yanayohusu maendeleo ya wananchi. Hivyo ni wajibu wa Chuo Kikuu cha Nelson Mandela kufanya utafiti katika maeneo muhimu yanayolenga katika kutatua matatizo yanayowakabili wananchi, likiwemo hili la upatikanaji wa maji chini ya ardhi. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na Taasisi, Vyuo, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Makampuni na watu binafsi wenye utaalam na vifaa, kufanya shughuli za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Kutokana na tatizo kubwa la maji katika Wilaya ya Muheza, Serikali ilipeleka fedha ili tuweze kuchimbiwa visima, lakini kwa bahati mbaya sana wataalam wetu waliruhusu kisima kichimbwe katika eneo lililokuwa halikufanyiwa utafiti na matokeo yake Taifa likaingia hasara kubwa.

(i) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wananchi wa Muheza juu ya wataalam waliosababisha Taifa kuingia hasara?

(ii) Katika utaratibu wa vijiji kumi kupatiwa maji kwa Mradi wa *World Bank,* Wilaya ya Mkinga imekidhi vigezo vyote lakini mpaka leo tunapozungumza ni kijiji kimoja tu kimefanikiwa kupatiwa fedha pamoja na kwamba tuna tatizo kubwa sana la maji. Serikali inawaambia nini wananchi wa Wilaya ya Mkinga? *(Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Kuhusu tatizo la Wataalam wa Halmashauri ya Muheza kuchimba visima ambavyo havikuwa kwenye utafiti, tumefuatilia tukagundua kwamba ni kweli katika vijiji tisa vilivyokuwa *earmarked* kuchimbiwa visima, viliweza kupatikana visima katika vijiji vitano. Moja ya vijiji hivyo ni Kijiji kinachoitwa Kilongo, ambacho mkandarasi aliyekwenda kuchimba kile kisima aliacha sehemu tatu ambazo zilioneshwa na wataalam kwa ajili ya uchimbaji akaenda kuchimba eneo lingine. Tumeongea na Mkurugenzi wamemwita mkandarasi na kukaa naye ili aoneshe michoro inayomthibitishia kuchimba eneo lile.

Ninachoweza kuagiza hapa ni kwamba, hii inaonesha dhahiri jinsi wataalam wetu, ukichukua mkandarasi halafu na yule mtaalam anayesimamia Halmashauri, kwanza kwa mkandarasi kuonesha kutofahamu umuhimu wa tafiti zinazofanywa kwa sababu siyo kila mahali panapochimbwa panaweza kuwa na maji kwa sababu ya kihaidrolojia. Kwa hiyo, alitakiwa kufuata zile sehemu ambazo yule mkandarasi aliyefanya utafiti naye afanye kwenye sehemu tatu mpaka nne.

La pili, inaonesha utovu wa nidhamu wa Msimamizi wa Halmashauri ambaye aliacha kisima kikachimbwa mpaka dakika za mwisho sehemu ambayo haipo kwenye mchoro. Nninachoagiza Halmashauri ya Muheza iweze kukaa na mkandarasi huyo na kama itathibitika kwamba ni kweli hakutumia michoro inayohusika kwenye sehemu husika, basi anawajibika kuchimba kisima kwenye Kijiji cha Kilongo kwenye maeneo yaliyokuwa yameainishwa na mtaalam. *(Makofi)*

Kuhusu Msimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Halmashauri inatakiwa imwajibishe kwa kufuata taratibu za kinidhamu kwa sababu alitakiwa asimamie na amwoneshe lile eneo kabla fedha za umma hazijatumika kiwango cha kumaliza halafu baadaye akalipwa wakati anafahamu kuwa hakufanya sehemu hiyo.

Mwisho, niwaombe Wataalam wote wa Halmashauri kusimamia kwa ukaribu Miradi hii ya uchimbaji wa visima vya maji na Miradi mingine kwa sababu tatizo kubwa la Miradi hii imeonekana ni usimamizi ambao ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sehemu ya pili ya swali, Vijiji Kumi vya Wilaya ya Mkinga kwa Mheshimiwa Kitandula, tunayo orodha ambayo inaonesha kwamba, kufikia tarehe 30 Mei, Halmashauri 60 ambazo zimeshakidhi vigezo vya Benki Kuu ya Dunia vimeshaidhinishwa kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji. Kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Kitandula, tuangalie kwenye orodha kama Mkinga ipo basi ni suala la kufuatilia, Mkurugenzi asaini mikataba na Wahandisi ili utaratibu wa ujenzi uweze kuanza. Ahsante.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Ninalo swali moja la Kisera. Ni ukweli kwamba Mradi wa Vijiji Kumi umecheleweshwa sana na utekelezaji wake umechukua muda mrefu na kila siku tunapewa taarifa za ahadi. Katika jimbo langu tulipangiwa vijiji vitatu, mpaka leo ni kijiji kimoja tu ndiyo kimeweza kufanikiwa kupata maelekezo ya kupata maji, wamechimba kisima hakina maji, hakuna taarifa yoyote, wataalam waelekezi wameondoka.

Serikali inatoa tamko gani kwa hivi visima kumi vya kila Wilaya ambavyo inaonekana tumeshindwa kabisa? Kwa nini Serikali haitoi tamko? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna tatizo la Miradi ya Vijiji Kumi na hasa kwenye uchimbaji wa visima na hasa pale inapoonekana visima vingi vilivyochimbwa havina maji. Yapo matatizo makubwa mawili; tatizo la kwanza kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi kwamba, siyo kila mahali unapochimba unatarajia kupata maji, kwa sababu tabia ya maji yanapatikana kwenye miamba maalum ambayo ina uwezo wa kuhifadhi maji na kusafirisha maji na wakati mwingine hiyo miamba inaweza ikawepo lakini kwa sababu za kihaidrolojia, maji lile eneo hayapo.

Vile vile tumesema wazi kwamba, mpaka sasa utafiti wa maji chini ya ardhi kwa teknolojia iliyopo ni kati asilimia 50 mpaka 70. Sasa la msingi hapa ni njia za utafiti ambazo inaonekana mpaka sasa sehemu nyingi bado utafiti wa kina haufanyiki kwa maana kwamba wale ambao wanakuwa wamepewa kazi ya kufanya utafiti, kwanza kabisa wanatakiwa waende kwenye mabonde ya maji kama Bonde la Pangani na kusoma taarifa za hali ya maji katika yale maeneo.

Sasa upungufu wa utafiti wa kina unasababisha kuwa na takwimu ambazo siyo sahihi, uchambuzi ambao siyo sahihi na maamuzi ambayo siyo sahihi na matokeo ndiyo wanachimba maji kwenye sehemu ambazo zinakuwa hazifai.

Ninachoweza kusema ni kwamba, kwa sasa yale maeneo ambayo uchimbaji umeonesha kwamba maji hayapo yakaingizwa kwenye awamu ya pili ya utekelezaji wa Miradi hii ya uchimbaji wa maji ya visima na mengine. Naendelea kusisitiza kwamba, kwa zile Halmashauri 60 kwa sababu mlolongo ulikuwa mrefu lakini sasa hivi tumeshafikia kiwango cha Halmashauri 60 ambazo zimeruhusiwa, basi wao wachukue hatua mara moja na kuanza kutekeleza hii Miradi na hasa kuzingatia kwamba fedha zote tayari zipo kwenye Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hii. *(Ahsante)*

Na. 14

**Hitaji la Umeme – Shule ya Sekondari ya Puma**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED HAMISI MISSANGA)** aliuliza:-

Shule ya Sekondari ya Puma ni miongoni mwa shule zilizoahidiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kujengewa maabara katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 lakini Shule hiyo haina umeme:-

Je, ni lini Shule hiyo itapatiwa umeme ili kuwezesha kutumika kwa maabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Puma ni miongoni mwa vijiji vilivyo na huduma ya umeme kwa muda mrefu sasa. Huduma hiyo ya umeme imeboresha maisha ya wananchi, kazi za uzalishaji na huduma za kijamii. Kutokana na uwepo wa huduma hiyo, Puma ina hospitali kubwa inayomilikiwa na madhehebu ya dini yanayotoa huduma bora Mkoani Singida. Serikali inatambua umuhimu wa maabara kwa Shule za Sekondari kwani bila umeme maabara yoyote haiwezi kutoa huduma au mafunzo yanayokusudiwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa huduma ya umeme ni matokeo ya mipango iliyoandaliwa mapema na *TANESCO* kwa kuzingatia uwezo wa bajeti ya shirika. Miradi ya kusambaza umeme kwa bajeti ya Shirika, huanza kutekelezwa kila mwaka kuanzia mwezi Januari na kuishia mwezi Desemba. Katika bajeti ya mwaka 2012, kwa Mkoa wa Singida, Mradi wa Kupeleka Umeme Shule ya Sekondari ya Puma si miongoni mwa Miradi iliyoombewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa huduma ya umeme katika Shule ya Sekondari ya Puma, Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO,* itaingiza Mradi huu kwenye maombi ya fedha ya bajeti ya Shirika kwa mwaka 2013.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa ni Sera ya Nchi kila sekondari lazima iwe na maabara; na kwa kuwa siyo rahisi kupeleka umeme kwa kila shule kwa muda mfupi; je, Serikali itakuwa tayari kuwekeza kwenye *solar* ili shule za sekondari nchi nzima ziweze kupata huduma ya umeme? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Miradi mingi ya Maendeleo inategemea sana miundombinu ya umeme; na kwa kuwa katika Kijiji cha Mwankoko Mradi wa Maji wa kupeleka Singida Mjini umeshakamilika kupitia *BADEA;* na kwa kuwa kikwazo imekuwa ni shilingi milioni 500 tu kufikisha umeme pale; je, Serikali itakuwa tayari sasa kupeleka umeme Mwankoko ili Mradi wa Maji uweze kukamilika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, anataka kujua kama Serikali tuna mpango gani wa kutumia njia mbadala ya umeme wa *solar* ili kuweza kuweka umeme katika shule zote za sekondari nchini. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi pale Wizarani tumejipanga na tupo kwenye tathmini mbalimbali za kuona ni gharama kiasi gani zinaweza zikafanyika kufikia maeneo yote ambako sekondari za kata zipo na shule za msingi. Gharama hizo na tathmini hizo zinaendelea kufanywa na wataalam wetu na tutakapokamilisha tutaweza kuleta taarifa na mapendekezo hayo. Kubwa hapa ni suala la fedha kwa ajili ya shughuli hiyo.

Kwa namna yoyote ile, napenda kuwaomba sana Watanzania kwa ujumla kwamba, hatutaweza kufikia nchi yetu kupeleka umeme kwa njia ya *grid* peke yake. Duniani huko, wenzetu njia ya *solar* ndiyo inayotumika kwa kiasi kikubwa; ni vyema tukafikiria na kupeleka mawazo yetu huko. Pia si vibaya kwa Halmashauri nazo kwa sababu *solar* zinajitegemea, kuwa na Miradi ya Maendeleo inayohusiana na masuala ya umeme hasa kupitia njia ya *solar* na wadau wengine wanaochangia masuala ya maendeleo. *(Makofi)*

La pili, ameuliza juu ya Kijiji cha Mwankoko; tunahitaji kiasi cha shilingi milioni 300 tu ili waweze kupata umeme. Nimhakikishie tu kwamba, tuwasiliane ili tuweze kuona namna ya kuingiza katika Miradi ya mwaka 2013 ili tuweze kuwapatia umeme katika sehemu hii. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya Shule ya Sekondari ya Puma inafanana kabisa na ile ya Sekondari ya Sanjaranda, Wilaya ya Manyoni. Je, Wizara itakuwa tayari kuiingiza shule hii katika mpango wake ili iweze kupata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Itakuwa ngumu kweli kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuweza kujua shule ilipo, lakini majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Lwanji, ambalo ameliuliza kuhusiana na sekondari iliyopo Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, *REA* wameonesha jitihada kubwa ya kufikia maeneo mengi, basi katika mipango inayofuata ya *REA* ni suala la mawasiliano ili tuweze kuona kama kweli na utafiti utakaofanywa na wataalam wetu ukithibitisha kwamba kweli kuna umuhimu huo, basi tunaweza tukajitahidi. Kama nilivyosema, njia ya *solar* pia inaweza ikatusaidia sana katika kupunguza matatizo ya maeneo ambayo hayajafikiwa na *grid*. *(Makofi)*

Na. 15

**Kudhibiti Uchimbaji Holela wa Madini ya *Uranium***

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE)** aliuliza:-

Madini ya *Uranium* ambayo yamegundulika kuwepo sehemu nyingi nchini ikiwemo Tunduru yana thamani kubwa sana, lakini pia ni hatari kwa maisha ya wananchi:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti uchimbaji holela wa madini hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa bado hatujafikia hatua ya uchimbaji wa madini ya urani, bali shughuli zinazoendelea hivi sasa ni za utafiti na uhakiki wa mashapo ili kuthibitisha kuwepo kwa mashapo ya kutosha yanayoweza kuchimbwa kiuchumi na kibiashara ili kubaini kama uwekezaji huo utaweza kufanyika. Hata hivyo, Serikali inaendelea kutumia Sera, Sheria na Kanuni za Madini zinazosimamia utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, usafirishaji na matumizi ya madini ili kuhakikisha kwamba, hakuna uchimbaji holela utakaoruhusiwa katika madini ya urani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kugundulika kwa madini ya urani katika maeneo kadhaa nchini yakiwemo ya Mto Mkuju, Namtumbo, Songea na Bahi, Manyoni hadi Itigi, Serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha kuwa kila atakayeomba leseni ya uchimbaji wa madini ya urani anaonesha ni namna gani atazingatia kanuni na Sheria za Usimamizi wa Sekta ya Madini zilizopo na kuzingatia miongozo/taratibu za Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomic *(IAEA)* za usimamizi wa madini hayo zitazohakikisha kuwa uchimbaji hauleti athari kwa watu na mazingira. Aidha, Serikali ina mikakati ya kujenga uwezo wa Wataalam wa Wizara kwa kiwango cha shahada za uzamili na uzamivu ili kuweza kusimamia utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini ya urani na pia uwezo wa kuingia mikataba itakayokuwa na manufaa kwa nchi.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri kabisa ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Amesema kwamba kutakuwa na utaratibu wa kuwawekea uwezo wafanyakazi; nataka kuuliza kwa sababu kazi ya kuchimba *uranium* ni nzito na hatuna wataalam wa kutosha.

Je, kazi hii itaanza lini na watapelekwa lini na mwaka upi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba wote tunafahamu kwamba madini haya ya urani ni madini hatari, lakini pia ni madini mazuri kwa matumizi ya shughuli mbalimbali za kimaendeleo. Sisi Wizarani tumetenga fedha ya bajeti katika bajeti hii, ikipata tu basi wataalamu hawa wataanza kwenda kusoma hizi shahada nilizozisema ili waweze kusaidia katika maendeleo ya kimkakati na maendeleo ya kudumu katika sekta hii ndogo ya madini ya urani.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naomba niulize swali fupi la nyongeza. Kwa sababu Serikali inatambua kwamba madini ya *uranium* ni hatari kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, nchi zilizoendelea na ambazo zimetumia madini ya *uranium* kwa ajili ya nishati kama Japan, zimepiga marufuku kabisa matumizi ya *uranium* katika kutengeneza umeme. Wajapani wamefunga mitambo 54 ya uzalishaji wa umeme, Ujerumani ina *faze-out* matumizi ya *uranium* katika kutengeneza umeme, sisi ambao ni maskini, hatuna kila kitu, tunaruhusuje *uranium* kuchimbwa katika nchi hii wakati hatuna uwezo kama walionao hawa ambao wanayakataa haya madini sasa hivi?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza lazima tuelewe kwamba sio kweli kwamba nchi hizi zimeacha kutumia *uranium* kuzalisha umeme, sio kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimsaidie Mheshimiwa Mbunge, nchi inayozalisha *uranium* kufuatana na swali la msingi, nchi ya kwanza duniani ni Kazastan, Kazastan haina wataalamu wengi kiasi hicho. Nchi nyingine ambazo zinazalisha zaidi ya kilo 1000 ni Canada, Australia na USA. Kwa hiyo, sisi kama Taifa ikiwa Kazastan ni ya kwanza, halafu hizi nchi kubwa tatu na zenyewe zinachimba na kuuza *uranium*, nadhani kama Taifa lazima tujue agenda yetu kwenye rasilimali zetu ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimsaidie vilevile kwamba katika nchi za Kiafrika, nchi ambazo zina *uranium* nyingi na zinachimba, ya kwanza ni Niger, ya pili Namibia halafu hata majirani zetu Malawi na mimi Malawi nimeenda mara nyingi, nimefanya utafiti nchini Malawi, Malawi haina wataalamu kutuzidi sisi na mgodi wao wa *uranium* ukifika pale Karonga, kama unaelekea kule chini Zomba, ukate mkono wa kushoto haiko mbali sana na hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu na isitoshe utumiaji wa umeme sio kweli, nchi kama Ufaransa asilimia 75 ya umeme wake unatokana na *nuclear*. Ujerumani na Japani, hata Japani yenyewe imejiuliza, usije ukachukua ile *accident* iliyotokea kwamba ndiyo inaweka *precedent* kwamba *uranium* haiwezi kutumika.

Halafu ndugu zangu, naomba nieleze kwamba nchi ya Kenya imetumia zaidi ya miaka saba kufanya utafiti na imeshapata *green light* kutoka *International Atomic Agency* na Kenya wana mkakati kwamba wakianza kuzalisha umeme wa *uranium*, sisi kama Tanzania tutakuwa soko lao. Kwa hiyo, ndugu zangu kama Taifa tusonge mbele. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hiyo ndiyo namna Professor Muhongo ametua ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara inayofuata, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, swali linatoka kwa Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

Na. 16

**Huduma kwa Watu wenye Ulemavu**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (K.n.y. MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA)** aliuliza:-

(a) Je, Tanzania ina wananchi wangapi wenye ulemavu?

(b) Kuna taarifa kuwa watu wenye ulemavu hupatiwa posho ya kujikimu. Je ni kiasi gani kwa mtu mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Sera ya Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002 na ongezeko la watu kwa asilimia 2.9 kwa mwaka, Tanzania inakadiriwa kuwa na watu milioni 43 na tukichukua usawa wa hesabu za uwiano kama ilivyoainishwa na Shirika la Afya Duniani *(WHO)*, kwamba mtu mmoja miongoni mwa kila watu kumi ni mwenye ulemavu. Hivyo basi, Tanzania inakisiwa kuwa na watu takribani milioni 4.3 kuwa ni wenye ulemavu. Hata hivyo tunategemea kupata takwimu sahihi zaidi katika zoezi la Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi litakaloendeshwa mwezi Agosti, 2012. Hivyo ninawaomba ndugu zangu wenye ulemavu na jamii

kwa ujumla kushiriki katika zoezi hili muhimu litakalowezesha kupata idadi sahihi ya watu wenye ulemavu ili kusaidia Serikali kupanga mipango ya jinsi ya kuwahudumia.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jamii yoyote kunakuwepo na kundi la watu ambao uwezo wao wa kujimudu kimaisha umepungua au haupo kabisa na hakuna mtu wa kuchukua jukumu hilo. Kutokana na hali hiyo, jamii husika inawajibika kutoa matunzo au msaada kwa watu hawa. Kulingana na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 inaelekeza kuwa jukumu la kutoa matunzo ya watu wenye ulemavu ni la jamii na kwamba familia ndiyo mhimili mkuu wa kuwatunza watu wenye ulemavu, utaratibu huu ni endelevu. Aidha, sera hiyo inaelekeza kuwa makazi ya watu wenye ulemavu yatakuwa kimbilio la mwisho baada ya mtu mwenye ulemavu asiyejiweza kukosa kabisa mtu wa kumtunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo hayo ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010, hakuna kipengele kinachoelekeza watu wenye ulemavu nchini kupatiwa posho ya kujikimu.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa wako walemavu wengi tu ambao hawana uwezo wowote wa kujikimu, je, Serikali inaziagiza nini Halmashauri na Manispaa kuhusu walemavu hao?

(b) Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kuwapatia posho hawa walemavu ili kuweza kujikimu na wao kujiona ni miongoni mwa watu wengine?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kama nilivyosema katika jibu la msingi, jukumu la kuwatunza watu wenye ulemavu ni jukumu la jamii, ni jukumu letu watu wenye ndugu na kwa naamna hiyo, siagizi Halmashauri kuanza kuwahudumia isipokuwa naagiza Halmashauri kutekeleza yaliyoainishwa katika Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 katika kuanza kuweka kumbukumbu ya watu wote wenye ulemavu ili waweze kutambuliwa katika Halmashauri zao na wale ambao watakuwa kabisa wamekosa mtu au jamii ya kuwahudumia waweze kupata matunzo katika maeneo maaalum yaliyotengwa kwa sababau hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la posho ni vigumu sana kwa Serikali kuanza kutenga posho kwa watu wenye ulemavu nchi nzima na ukichukua ongezeko la watu, kadiri tunavyokuwa tunaongezeka ndivyo asilimia ya watu wenye ulemavu inavyoongezeka. Ni jambo muhimu zaidi kuweza kutengeneza mazingira ya watu wenye ulemavu kumudu maisha yao kama ilivyoainishwa katika Sera ya mwaka 1984 na iliyoainishwa katika Sheria yetu ya mwaka 2010 pamoja na Kanuni zake. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nakuona Mheshimiwa Kamishna lakini kwa sababu ya muda, naomba tusonge mbele. Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mbunge wa Masasi, aulize swali linalofuata.

Na. 17

**Ukarabati wa Chuo cha Wasioona - Mtapika**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Katika bajeti ya mwaka 2011/2012, Serikali iliahidi kufanya ukarabati wa Chuo cha Wasioona cha Mtapika kilichopo Masasi:-

(a) Je, kwa nini hadi sasa ukarabati huo haujafanywa na fedha zilishatengwa?

(b) Je, fedha iliyotengwa imefanya kazi gani na wapi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe kama ifautavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mpango wa kukarabati Vyuo vya Watu Wenye Ulemavu nchini ikiwemo Chuo cha Ufundi cha Wasioona cha Mtapika, Masasi katika bajeti yake ya mwaka 2012/2013 pamoja na Chuo cha Ufundi Masiwani, Tanga; Chuo cha Wanawake Wasioona, Singida; Chuo cha Luanzari, Tabora na Chuo cha Ufundi, Yombo, Dar es Salaam. Vilevile, Wizara haikutenga fedha kwa ajili ya kukarabati Chuo cha Wasioona cha Mtapika katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Ukarabati wa Chuo hiki umetengewa fedha katika bajeti ya mwaka huu wa 2012/2013 ambapo kesho itakuwa inawasilishwa ili kazi hiyo iweze kutekelezeka. Tumetenga kiasi cha Tshs. Milioni 500 ambazo zitatumika katika ukarabati wa Chuo cha Ufundi Masiwani Tanga, Chuo cha Wanawake Wasioona Singida, Chuo cha Luanzari Tabora, Chuo cha Ufundi Yombo, Dar es Salaam pamoja na Chuo cha Mtapika, Masasi.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu imeamua kujenga vyuo vya *VETA* kila Wilaya na kwa kuwa majengo haya ninayoyazungumzia yamekaa zaidi ya miaka kumi bila matumizi yoyote, je, Wizara haioni ni busara kukabidhi majengo haya kwa ofisi ya Waziri Mkuu ili aweze kupewa kibali cha kubadilisha matumizi, kiwe Chuo cha VETA ili kiweze kuwasaidia vijana wetu wa Masasi wanaomaliza masomo na kukosa nafasi za kuendelea?

(b) Kwa kuwa katika Chuo hiki bado kuna wafanyakazi ambao wamekaa zaidi ya miaka kumi na hawafanyi kazi yoyote lakini wamekuwa wakilipwa mishahara, je, Serikali haioni iko haja ya kuwapatia uhamisho Walimu hawa wakaenda katika vyuo ambavyo vinafanya kazi kuliko kuendelea kuwaacha pale wakikaa bila kazi ya aina yoyote na Serikali kuendelea kuwalipa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kubadilisha matumizi hatulioni kwamba ni la busara sasa kwa sababu Chuo hicho kinatumika kwa ajili ya kuwapatia mafunzo watu wasioona na tumetenga fedha kwa ajili ya kukifanyia ukarabati na hivyo kukiboresha ili kiweze kutoa msaada zaidi kwa wale wenzetu wasioona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wafanyakazi kwamba wapo ambao hawana kazi, naomba baada ya kumaliza hapa tuwasiliane ili niweze kuwafahamu wafanyakazi hao wana sifa gani ili tuweze kuangalia namna muafaka ya kuweza kuwatumia wataalamu hao vizuri.

Na. 18

**Utekelezaji wa Sheria kwa Haki**

**MHE. JAMES F. MBATIA (K.n.y. MHE. AGRIPINA Z. BOYOGERA)** aliuliza:-

Katika hali ya kawaida inayofuata misingi ya Haki na Usawa hakuna mtu yeyote katika nchi hii aliyekuwa juu ya Sheria; lakini kumekuwa na hali ya kuwaonea aibu watu wenye nacho kuwachukulia hatua za kisheria na wanyonge kucheleweshwa kuchukuliwa hatua za kisheria inapowapasa hivyo mara moja hata kama kosa lake ni kama lile la mwenye udhaifu:-

(a) Je, Serikali inasema nini katika mazingira kama haya?

(b) Je, katika mazingira kama hayo, Mbunge ambaye ni mwakilishi wa wananchi anastahili kuchukua hatua gani anapobaini hali kama hii katika utekelezaji wa Sheria?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria na kwa misingi hiyo hakuna mtu aliye juu ya sheria. Hivyo Serikali kupitia vyombo vya dola yaani Mahakama, Polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inawajibu na inafanya kila liwezekanalo kuhakikisha Sheria zinafuatwa na kutekelezwa na watu wote kwa usawa na kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaokiuka sheria zilizowekwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ambaye ni mwakilishi wa wananchi anapobaini kukosekana kwa usawa katika kuwashughulikia wanaokiuka Sheria, ana wajibu wa kuwasiliana na vyombo vya dola na asasi nyingine zinazojihusisha na masuala ya kisheria na haki za binadamu ili tatizo husika liweze kushughulikiwa. Aidha, Serikali ipo tayari kupokea malalamiko yoyote yatakayowasilishwa kwake na Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuhusu ucheleweshwaji wa kuchukua hatua za kisheria dhidi ya yeyote anayekiuka sheria. Isitoshe ni vyema Mheshimiwa Mbunge akatambua kuwa yeye ni mlinzi wa amani, hivyo dhamana yake katika kuhakikisha nchi inafuata utawala wa sheria ni kubwa sana na ni sawa na walinzi wengine wa amani waliopo nchini.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri hapa ambayo kwa kiasi kikubwa yanakinzana na dhana nzima ya haki za binadamu ukizingatia kwa mujibu wa Katiba yetu, Ibara ya 9, kifungu cha F tumeridhia Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu ambalo limeagiza nchi zote wanachama waweze kutoa kanuni hizi kufundishwa katika mashule na taasisi zote zinazoendesha masuala ya elimu, sasa swali:-

(a) Je, ni kwa kiasi gani agizo hili la Baraza la Mataifa au *Universal Declaration of Human Rights* limetekelezwa hapa kwetu Tanzania kwenye taasisi zinazotoa elimu?

(b) Kwa kuwa swali la utoaji wa haki za binadamu kule Kasulu Vijijini hasa Kata ya Rungwe Mpya na Eruishingo limekiukwa kwa kiasi kikubwa na ndiyo msingi wa swali la msingi, Watendaji wa Kata na Vijiji huwanyanyasa wale ambao hawako kwenye mamlaka za kwao, za Kiserikali. Je, Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Mambo ya Ndani, wanatamka nini hapa kwa kuwa, Serikali inafanya kazi kwa pamoja, ili wale watendaji wote waliokiuka haki hizi za msingi za binadamu, ukichanganya na hivi majuzi Tandahimba na kule Rufiji, haki zao zinafanyiwa nini?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbatia, kwa kuteuliwa kwake kuwa Mbunge katika Bunge lako Tukufu. Naomba nijibu maswali yake mawili ya nyongeza, ambayo hayahusiani na swali la msingi, kama ifuatavyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Universal Declaration of Human Rights,* kweli imetolewa na sisi tumeiridhia na kwa kiasi kikubwa tumetekeleza mengi sana yaliyomo ndani ya *Declaration* ile. Kila wakati tunapotakiwa tunapeleka kitu kinaitwa *Periodic Review Report* na mwaka jana tumepeleka ripoti yetu ya utekelezaji wetu wa Azimio lile la Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ni suala tu la tumefundisha nini katika shule zetu, nasema bado ni utaratibu, tutaendelea nao, tuta-*introduce* suala la *Human Rights* kwenye shule zetu. Lakini kwenye vyuo, hasa Vyuo Vikuu, suala hili linafundishwa. Sasa labda turudi mpaka shule za kule Kasulu, tutafika huko japo tutachukua muda, lakini tutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya nchi hii, kwa kweli katika nchi ambazo zimesifiwa kuzingatia utekelezaji wa haki za binadamu, Tanzania ni mojawapo; tumesifiwa sana na kwa kweli tunafanya vizuri sana. Matukio machache yanayotokea, ukizungumzia Songea, ukizungumzia wapi yanatokea, lakini linganisha hayo na yanayotokea nchi nyingine, utaona jinsi ambavyo sisi tuko mbali sana, hatutaki yatokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki za binadamu kule Kasulu, hili ni *very specific,* ningepewa *incidences* ambazo ni *specific,* naomba nizipate, ili sisi tuzishughulikie. Tunayo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo ingeweza kabisa kufika kule. Imefika sehemu nyingi, ingepata hizo *cases* za Kasulu, tungeweza kuwatuma na nitamwomba Mheshimiwa Mbunge anipatie, kwa kweli tungependa kuzifuatilia, ili tupate ufumbuzi wa jambo hilo.

Na. 19

**Hitaji la Kivuko Mto Songwe**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MHE. ALIKO N. KIBONA)** aliuliza:-

Nchi za Tanzania na Malawi zimekuwa na ushirikiano mzuri katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kibiashara na wakati mwingine katika mambo ya misiba. Mpaka wa nchi hizi mbili ulioko upande wa Ileje unatenganishwa na mto mkubwa wa Songwe ambao ni hatari kwa watumiaji wa kivuko hicho:-

Je, Serikali itakuwa tayari kujenga kivuko kwenye mto huu ili kunusuru maisha ya raia wetu na mali zao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imepokea ombi la Mheshimiwa Mbunge. Aidha, kabla ya Serikali kufikia uamuzi wa kujenga kivuko kwenye Mto Songwe, Wizara itatuma wataalam katika mwaka wa fedha 2012/2013 ili kutafiti uwezekano wa kujenga kivuko. Utafiti huo utajumuisha kina cha maji cha kutosha kivuko kuelea wakati wote wa masika na kiangazi pamoja na upana wa mto eneo litakaloonekana linafaa kuweka kivuko. Matokeo ya utafiti huo ndiyo yataiwezesha Wizara kufanya uamuzi wa kujenga kivuko hicho au kutojenga.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la Mheshimiwa Waziri pale au la Serikali, liko juu juu sana. Naomba kwa kuwa, mto huo unatishia maisha ya watu pale pindi wanapovuka kuelekea ng'ambo, naomba Serikali iji-*commit* ni lini kwa kweli, watafiti hawa watakwenda? Ni mwezi unaokuja mwaka huu? Naomba nithibitishiwe hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanjale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi ni kwamba, huwezi kuweka kivuko kabla hujafanya utafiti. Nimeahidi kwamba, katika Mwaka wa Fedha huu ambao ndio bajeti mtaipitisha, tutapeleka Wataalam wakafanye utafiti waweze kuona ni wapi panafaa kuweka kivuko, wanaangalia kina cha maji na upana. Hiyo kazi ni lazima ifanyike kabla ya kusema lini kazi ya ujenzi hasa ingeweza kuanza.

Na. 20

**Ujenzi wa Barabara ya Kibiti – Lindi**

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Barabara ya Kibiti – Lindi ni kiungo cha nchi za Malawi, Msumbiji na Afrika ya Kusini kwa biashara ya utalii na ujirani mwema, lakini ujenzi wake unasuasua:-

(a) Je, ujenzi wa barabara hiyo utamalizika lini?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kutokamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo, iliyochukua kipindi kirefu tangu mwaka 1974 hasa ikizingatiwa kuwa kunaweza kuwa na mvua nyingi sana mwaka huu ambapo mara nyingi zimekuwa zikiathiri sana barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kibiti – Lindi hadi Mingoyo yenye urefu wa kilometa 344 imekuwa ikijengwa kwa kiwango cha lami hatua kwa hatua, yakiwemo madaraja ya Mkapa, Mbwemkuru, Matandu, Mavuji na mengineyo, ambayo yalikuwa ni kikwazo kwa usafiri wa barabara hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa kilometa 284 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na kubakia kilometa 60 za Ndundu – Somanga, ambapo hivi sasa Mkandarasi M/S M.A. Kharafi anaendelea na ujenzi wa sehemu hiyo kwa gharama ya shilingi bilioni 59, ambayo imepangwa kukamilika katika mwaka wa 2012/2013. Hadi sasa hivi, Mkandarasi amelipwa shilingi bilioni 45.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, itaendelea kusimamia kazi ya ujenzi wa sehemu ya barabara iliyobaki na kuhakikisha inakamilika mapema iwezekanvyo. Aidha, ni jukumu la Mkandarasi, Kharafi, kuifanyia matengenezo barabara hiyo na kuhakikisha kuwa, inapitika wakati wote.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imesumbua sana, sasa ni takriban miaka 38 na watu wote wanafahamu. Nataka Serikali itambue kwamba, watu wa Kusini Mtwara, Lindi, Ruvuma, wanapata adha kubwa sana kwa kutokamilika barabara hii, la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunataka sasa tufahamu kwa sababu, swali kama hili liliulizwa miezi mitatu ya nyuma, tukaambiwa kwamba, baada ya siku 180 barabara itakuwa imekwisha, lakini mpaka sasa bado haijakwisha. Tunaomba sasa Serikali, ituambie tena tujue ahadi zetu na hesabu, ituambie tena inakwisha lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikubaliane na wewe kwamba, wananchi kweli kwa sehemu hiyo ya Ndundu – Somanga wanapata adha kwa sababu, barabara ile haijakamilika. Lakini nikupe majibu ya kutia moyo ni kwamba, kazi inayoendelea sasa hivi katika hizo kilometa 60, kilometa 20 tayari wameshaweka lami. Pia nikuhakikishie katika Mwaka wa Fedha huu unaokuja wa 2012/2013, barabara hiyo itakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Waheshimiwa Wabunge. Kama mtakavyoona muda wetu wa Kipindi cha Maswali umekwisha, naomba nianze na matangazo ya wageni tulionao katika Ukumbi wetu.

Tunaye Dokta Mwamba, kwenye *Gallery* ya Spika, ambaye ni Naibu Gavana wa Benki Kuu; karibu sana Dokta Natu Mwamba. Pia yupo Dokta Ad KoekKoek, Balozi wa Uholanzi hapa

nchini, ambaye ameambatana na Afisa anayehusika na Masuala ya Siasa, Bi Agnes Hanti; naona hawapo hawa. *(Makofi)*

Pale *Gallery* ninao wageni maalum, Wilaya ya Kongwa ni moja ya Wilaya isiyokuwa na wasomi kwa miaka mingi, lakini kwa mara ya kwanza tunao vijana karibu sita wako Chuo Kikuu cha *UDOM* na wamenitembelea leo, naomba wasimame. Yupo Loy Kusenha, Neema Patrick, Lekuchela Mengi, Mwaluko Philimon, Ulanga Ulanga, Chibago Yona, Karibuni sana Bungeni. Anayesema hakuna maendeleo nchi hii, mchawi. *(Makofi)*

Wageni waliofika kwa ajili, ya mafunzo Bungeni ni wanafunzi 91, kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma*,* ushuhuda mwingine huo. Karibuni sana vijana wetu wa *UDOM,* ni Bunge lenu hili, ni vizuri sana kutumia fursa hii kujifunza na kuona namna ambavyo chombo hiki muhimu sana katika nchi yetu kinavyofanya kazi, karibuni sana. *(Makofi)*

Matangazo ya Vikao, kwanza ni Kamati ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mama Margreth Sitta, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa 8.00 Mchana, Ukumbi 231, Ghorofa ya Pili.

Vile vile Kamati ya Sheria Ndogo, ikutane Ukumbi Namba 219 baada ya kuwa tumeahirisha shughuli za hapa..

Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Juma Nkamia, anawaomba mkutane baada tu ya kipindi hiki, tutakapokuwa tumeahirisha hapa, Ukumbi wa Msekwa B. Halafu, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa David Homeli Mwakyusa, Mwenyekiti wake, anaomba mkutane Ukumbi 227 mara baada ya hapa.

Halafu kuna Tangazo moja muhimu sana, Wabunge wote wa *CCM,* saa 10.00 jioni, kutakuwa na Kikao Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, pamekuwa na baadhi ya Wabunge, ambao tayari wameanza kuleta karatasi zao za kuomba kuchangia baadhi ya Hotuba za Bajeti za Wizara mbalimbali. Tunatambua kabisa uharaka walionao Waheshimiwa Wabunge, kwa kuanza kuleta maombi hayo kwa ajili ya kuchangia hotuba hizo. Lakini niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunayo *Speaker's Ruling* hapa, Mheshimiwa Spika, Anne Makinda, aliwahi kutoa *Ruling* hapa; lakini vilevile kwa kuzingatia uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na kwa kipindi hiki ambacho ni kirefu tunachokiendea, ni lazima tupange mambo yetu vizuri. *(Kicheko)*

Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 60 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, maombi hayo yanatakiwa yawasilishwe Hoja inapokuwa imewasilishwa Mezani. Kwa msingi huo, maombi yataanza kupokelewa kesho tarehe 14 Juni, 2012 na kwa hiyo, wale wote waliokwishawasilisha maombi yao mapema kabla ya wakati huo, wahesabu kwamba, maombi yale yamefutwa. *(Makofi)*

Tunaomba tuzingatie sana utaratibu huo, ili pasitokee malalamiko baadaye ya kwamba, mtu aliwasilisha mapema lakini jina lake halikujitokeza. Lakini tukumbuke vilevile Waheshimiwa Wabunge, kuwahi katika kuwasilisha maombi kwa sababu, wakishawahi wenzako, ukaja mwishoni ukikosa nafasi usilalamike.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba, *Order Paper* yetu ya leo, tutamaliza shughuli muda mfupi ujao kwa sababu, tunajaribu kutoa nafasi kwa baadhi ya Kamati ambazo hazijamalizia malizia baadhi ya mambo, katika kujiweka sawa kwa safari tunayoiendea ya kushughulikia bajeti, ziweze kufanya hivyo.

Mwisho basi, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote, mlioteuliwa na Mheshimiwa Rais, kushika nafasi zenu na tunawahakikishia ushirikiano mwema kabisa na tunawatakia Waheshimiwa Wabunge wote, kila la heri katika kipindi hiki cha bajeti ambacho kitatuchukua mpaka mwezi wa Agosti katikati. Tunatarajia ushirikiano wa kila aina kabisa. Tunawaomba wananchi wa hapa Dodoma, watoe

ushirikiano kwa Waheshimiwa Wabunge, ili waweze kuishi kwa salama kabisa kwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Katika kumalizia malizia, nilipata vijikaratasi vingi hapa vya Waheshimiwa Wabunge, lakini mengine ngoja niyaache. Wanakumbushia kumbushia vidonda kule Uwanja wa Taifa. Natumaini tumeelewana.

**WABUNGE:** Hatujaelewana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge; aah, hatujaelewana tu? Wale wapenzi wa ile timu nyingine wanasema kwamba, wataendeleza kile kipigo cha mabao matano matano. *(Makofi/Kicheko)*

Basi, baada ya kufikia hapo Waheshimiwa Wabunge, naomba ...

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Looh, ni mmoja tu, eeh?

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Looh, ni mmoja tu, eeh?

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Kangi?

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniwie radhi, naomba Mwongozo chini ya Kanuni ya 68 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuonekana kwamba, Taasisi hii muhimu imekuwa ikituhumiwa kwa mambo ya kudai na kupokea rushwa, naomba nirejee Mkutano wa Tano, Mheshimiwa Mkulo, akiwa Waziri wa Fedha kwa wakati huo, vile vile aliwahi kuituhumu Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwamba, imehongwa na *CHC* na ndio maana wanaitetea kwa uchungu na hisia kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo huu kwa sababu, mpaka leo kumbukumbu zinaonesha kwamba, Kamati ya Hesabu za Mashirika Umma ilihongwa na alitaja hata idadi ya fedha kwamba, ni milioni 60. Mheshimiwa Zitto Kabwe, aliweka rehani Ubunge wake endapo itathibitika na yeye mwenyewe akasema kwamba, *CAG* amemwagiza aweze kufanya uchunguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile katika Mkutano wa Saba wa mwezi wa Nne katika mchango wangu, pia nilimwomba Waziri Mkulo, ama afute kauli yake kwa kuweka kumbukumbu sawa au alete ushahidi, kwa bahati mbaya hakuwepo. Kwa vile leo Mheshimiwa Mkulo yupo, ili usije umma ukawa unadhani kwamba, katika Bunge hili kumekuwa na mambo ya rushwa rushwa yanatajwatajwa bure, wakati mwingine pia huwa tunakataa jina la Mungu lisitajwe bure, sasa hivi mambo ya rushwa yanatajwatajwa tu kwa kusingizia; Taasisi hii inasingiziwa mambo mengi sana ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba utoe Mwongozo, Mheshimiwa Mkulo, afute kauli yake, ili kuitendea haki Kamati hii na Bunge hili ama alete ushahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba kusema kwamba, nimelipokea jambo hili. Nitalitolea Mwongozo kwa wakati muafaka.

Kwa hatua hiyo Waheshimiwa Wabunge, naomba kuahirisha shughuli za Bunge, hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.21 Asubuhi, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 14 Juni, 2012, Saa 3.00 Asubuhi)*